





Kujifungua

Å føde


-  LIDA Norge
-  Sara Dorteia Johannesen
-  Jacob Haule
-  4
-  Kiswahili sw / norsk nb



Selamawit ana umri wa miaka 29. Alimzaa mwanee wa kwanza nchini Eritrea. Yeye na familia yake walikuwa na maisha magumu huko, kwa hiyo wakaamua kwenda Italia.

• • •


Selamawit er 29 år. Hun fødte sitt første barn i Eritrea. Hun og familien hadde det vanskelig der, så de bestemte seg for å dra til Italia.



Inga aliondoka nyumbani kabla hajafikisha miaka 19.
Alienda Norwei na akapata mwanee wa kwanza huko.

. . .


Inga dro hjemmefra like før hun fylte 19. Hun flyttet til
Norge og fikk det første barnet sitt der.



Wakati Selamawit alipopata ujauzito wa mtoto wake wa pili, alistaajabu jinsi itakavyokuwa kujifungua mtoto katika nchi tofauti.

• • •


Da Selamawit ble gravid med det andre barnet sitt, lurte hun på hvordan det ville være å få barn i et annet land.



Selamawit na Inga wana tajiriba tofauti. Selamawit alihisi yuko salama kwa sababu ana uzoefu wa kujifungua. Inga alizungumza na mama yake kuhusu kujifungua.

. . .


Selamawit og Inga hadde ulik bakgrunn. Selamawit følte seg trygg fordi hun hadde erfaring med å føde. Inga snakket med moren sin om å føde.



Wanawake wote wawili walifahamu kwamba katika mataifa mengi ya Ulaya, wanawake wajawazito wana haki ya kupata huduma za afya. Hii inamaanisha kwamba watapata msaada wakati wa ujauzito wao. Selamawit alipanga miadi na daktari wake mara tu baada ya kugundua kuwa ni mjamzito. Mume wa Selamawit alimpeleka kwa daktari.

. . .


Begge kvinnene hadde hørt at i de fleste europeiske land har gravide rett til svangerskapskontroll. Det betyr at man får hjelp under svangerskapet. Selamawit bestilte en time hos legen sin så snart hun skjønte at hun var gravid. Mannen til Selamawit kjørte henne til legen.



Daktari alifanya baadhi ya vipimo na akagundua kuwa Selamawit ana aina fulani ya kisukari ambacho wanawake wengi wajawazito hupata. Alipaswa kula vyakula vyenye virutubisho na kufanya mazoezi. Selamawit alifurahi kwani alienda kwa daktari mapema kabla yeye na mtoto wake kuugua.

. . .


Senere tok legen noen prøver og fant ut at Selamawit hadde en type diabetes som noen gravide kvinner får. Hun måtte spise sunn mat og trene. Selamawit var glad hun dro til legen tidlig, før hun og babyen ble syke.



Baada ya jirani wa Inga kusikia kwamba anajaribu kupata mtoto, akamshauri amuone daktari mara tu baada ya kugundua kuwa ni mjamzito. Kwa kufanya hivyo, angeweza kuwa na uhakika kwamba yeye na mtoto wake wangekuwa na afya njema. Daktari akamwambia anywe vidonge vya wajawazito vina vitamini muhimu kwa wanawake wajawazito.

. . .


Da naboen til Inga hørte at hun prøvde å få barn, sa naboen til henne at hun måtte gå til legen så snart hun ble gravid. På den måten kunne hun være sikker på at hun og barnet var friske. Legen sa at hun måtte ta folsyre, et vitamin som er viktig for gravide.



Inga na daktari wake walikubaliana kwamba aonane na mkunga kwa ajili ya vipimo vya mara kwa mara wakati wote wa ujauzito. Mkunga alimpa ushauri kuhusu chakula, kupumzika, na taarifa za jinsi ya kujilinda vizuri yeye na mtoto wake.

...

Inga og legen hennes ble enige om at hun skulle møte en jordmor for jevnlig oppfølging under svangerskapet. Jordmoren ga henne råd om mat, hvile og informasjon om hvordan hun selv og babyen kunne holde seg sunne og friske.



Wanawake wote wawili walijifungua watoto wenye afya bora. Selamawit alipata mtoto mwingine wa kiume wakati Inga alipata mtoto wa kike. Waume zao walihisi fahari na walimwambia kila mtu waliyemjua kuhusu wake zao imara na watoto wao wenye afya bora.

...

Begge kvinnene fødte sunne og friske barn. Selamawit fikk en sønn til, mens Inga fikk en datter. Mennene deres var veldig stolte, og de fortalte alle de kjente om de sterke konene og de friske barna sine.



LIDA Stories

lidastories.net

Kujifungua

Å føde



LIDA Norge



Sara Dorthea Johannesen



Jacob Haule (sw), Espen Stranger-Johannessen (nb)

